

SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Simu: 2133990

Telegramu: Railways

Nukushi: 2133428



Ofisi ya uhusiano

S.L.P 76959

Dar es Salaam

TAARIFA KWA UMMA KUONGEZeka KWA SIKU ZA SAFARI ZA TRENI YA ABIRIA DAR ES SALAAM – KILIMANJARO

Dar es Salaam, Desemba 12, 2019

Shirika la Reli Tanzania - TRC linawatangazia wateja wanaotumia huduma ya usafiri wa reli nchini, kuongezeka kwa idadi ya siku za safari kwa treni ya abiria kutoka Dar es Salaam kuelekea Moshi mkoani Kilimanjaro, Kutokana na maombi ya uhitaji wa wateja juu ya usafiri wa treni ya abiria kuanzia siku ya Jumatatu Desemba 16, 2019.

Awali treni ya abiria ilikuwa ikifanya safari kati ya Dar es Salaam na Moshi tangu tarehe 6.12.2019 mara nne kwa wiki, ambapo ilikuwa ikitoka Dar es Salaam siku ya Jumanne na Ijumaa, na kutoka Moshi siku ya Jumamosi na Jumatano. Shirika limefanyia kazi maombi ya wateja kwa kuongeza idadi ya safari za treni kuwa mara sita kwa wiki.

Treni ya abiria itakua ikianza safari kutoka Dar es Salaam kwenda Moshi siku za Jumatatu, Jumatano na Ijumaa Saa 10:30 Alasiri na kutoka Moshi kuelekea Dar es Salaam siku za Jumanne, Alhamisi, na Jumamosi Saa 10:30 Alasiri.

Shirika linawashukuru wateja kwa kuonesha kufurahia huduma za usafiri wa treni ya abiria mkoani Kilimanjaro ambao ulisimama kwa takribani miaka 26 na kuonesha ushirikiano katika kipindi cha ukarabati wa miundombinu ya reli Daresasalam – Moshi. Sambamba na hilo Shirika linawaomba wananchi kuendelea kutoa ushirikiano ili kuhakikisha miundombinu ya reli inakuwa salama muda wote ili kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji nchini.

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Jamila Mbarouk'.

Imeandaliwa na Mkuu wa kitengo cha Uhusiano TRC

Jamila Mbarouk